

# **WILAYA YA MARAKWET MAGHARIBI**

## **102/1**

### **KISWAHILI**

#### **Karatasi 1**

#### **MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

1. (a) Barua iandikwe kwa muundo wa barua rasmi. Iwe na:
- Anwani ya mwandishi sehemu ya juu mkono wa kulia.
  - Tarehe chini ya anwani ya mwandishi.

-Anwani ya mwandikiwa (Mhariri) upande wa kushoto baada ya ile ya mwandishi.

-Mtajo

-mada/mint/kuh.

- Mwili

-Sahihi

-Jina la mwandishi

>Mtahini asipozingatia muundo aondolewe alama 4 za sura.

- b) Hoja za maudhui

-Haki za kibinadamu zimepewe kipaumbele

-Kuwepo ugavi sawa wa raslimali za kitaifa

-Usawa wa kijinsia kutiliwa maanani.

-Uhuru wa kupata uraia wa nchi mbili

-Kuhakikisha utawala bora na uwajibikaji mionganoni mwa viongozi

-Kuangazia kwa suala la maadili na uongozi bora.

-Kuimashwa kwa taasisi za kisheria za kushughulikia masuala ya kijamii na kitaifa k.m

Tume ya usawa na jinsia, Tume ya kuwaajiri wafanyakazi wa umma n.k

2. Njia za kustawisha michezo nchini.

Vidokezi

-wanamichezo waajiriwe na serikali

-waalimu wa michezo wawe wamehitimu

-vipawa vya wanamichezo vitambuliwe mapema.

-vyuo maalumu vya michezo vianzishwe nchini

-kufanya somo la michezo kuwa la lazima nchini.

-kuondoa siasa michezoni.

-wachezaji na wasimamizi wapewe motisha

-wanamichezo wastaafu wapewe heshima

-pawe na bima ya kushughulikia wanaoumia

-vifaa vya michezo visitozwe ushuru

-kuwe na vifaa vya kutosha na vya kufaa.

Kutuza

Insha kamili iwe na hoja zisizopungua tano na zifafanuliwe.

3. Hii ni insha ya methali

Mwanafunzi atunge kisa na kioane na methali. Kisa kidhititishe ukweli kwamba mtu

hukidharau kitu au chombo alichotumia kuvukia mahali fulani.

Methali hii huweza kutumiwa katika muktadha ambapo mtu fulani amemtenda mwingine hisani au wema fulani kisha akaishia kudharauliwa na aliyemfadhili au kumtenda wema huo.

Tazama:

-Si lazima mtahiniwa aandike kichwa.

-maelezo ya maana ya nje au ya ndani yasipoafikiana katika utangulizi ni kosa dogo la maudhui.

-Si lazima mtahiniwa atangulize insha kwa kueleza maana ya nje au ya ndani ya methali.

Tafsiri yake ya methali ikiwa sawa lakini kisa kisithibitishe ukweli wa methali hii atakuwa amepotoka kimaudhui - 03

-Anayenakili kichwa na kukosa kushughulikia swali atachukuliwa kuwa amejitungia swali lake na kulijibu (BK 01= D-01)

-Ni sharti mtahiniwa ashughulikie pande mbili za methali.

4. Hii ni insha ya mdokezo. Huu ni mdokezo wa kumalizia.

Mtahiniwa aandike inshajinsi alivyoshuhudia yale anayodokeza.

-Kisa kitakachosimuliwa kionyesha tukio au hali ya kusikitisha inayoweza kumfanya mtu alie k.m tukio lililosababisha maafa makubwa.

- Kisa kisichoafikiana na mdokezo kituzwe alama 03 kwani mtahiniwa atakuwa amepotoka.

# **WILAYA YA MARAKWET MAGHARIBI**

102/2

## **KISWAHILI**

### **Karatasi 2**

#### **MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

##### **UFAHAMU**

- (a) Mwaka 1996 wakati kamati ya uraibu ya wazara mbalimbali ilipoundwa. (1 × 2)=2
- (b) Azma (lengo) kuanzisha kampeni ya uhamasisho wa umma dhidi ya dawa za kulevyta hasa mionganoni mwa vijana (1× 2)=2
- (c) Wajibu(majukumu) yalizidishwa kujuuisha  
(i) kutoa lseni kwa vituo vya kutibu waadherewa.  
(ii) kusimamia sheria na sera za kusitisha usambazaji wa dawa za kulevyta .  
(iii) kusaidia serikali za kaunti kusitisha usambazaji wa dawa za kulevyta.  
(iv) kuwasilisha ripoti bungeni kuhusu udhibiti wa dawa za kulevyta.
- Hoja zozote (3 × 1)=3
- (d) (i) Hawezi kishiriki katika ujenzi wa taifa  
(ii) Hawezi kushiriki katika shughuli za kuleta maendeleo katika elimu,uhifadhi wa mazingira,ukulima,usalama n.k.
- Hoja (2 × 1)=2
- (e) Ndio imefaulu kwani imeweza kuyafikia baadhi ya makundi k.v  
-wanaojidunga sindano  
-madereva  
-vijana katika mitaa duni  
-wanaopitia tambiko za kitamaduni  
-wahudumu wa matatu na bodaboda  
-walemvu
- Kutaja makundi mawili (2 ×1)=2
- (f) Maana ya methali ni kwamba hakuna jambo ambalo daima lina ukamilifu pekee.  
Hukabiliwa na changamoto za hapa na pale.
- Maelezo (1× 1)=1
- Juhudi (kampeni) za NACADA zinakabiliwa na changamoto tele:  
(i) Viwango vya juu vya bidhaa hizi za kulevyta.  
(ii) Mbinu hafifu za kuukomesha uraibu.  
(iii) Vileo vingine havijadhibitishwa kisheria  
(iv) Kimya na kukana kuwepo kwa tatizo hili  
(v) Hakuna huduma za kutosha za matibabu  
(vi) Wadau kuingilia kampeni kupitia mahakama  
(vii) Matangazo yasiyo na maadili
- Hoja zozote (2 × 1)=2
- (g) Mwongo – kipindi cha miaka kumi.(10)
- (1× 1)=1

#### **2. MUHTASARI**

- (a) -watoto milioni kumi hufariki kila mwaka kabla ya miaka 5.  
-vifo hivi hutokana na magonjwa  
-wengi wanaweza kuokolewa wazazi wakihudhuria kliniki.  
-kliniki hutoa chanjo,mawaiidha na mwongozo wa malezi  
-kipindi cha miaka mitano ya kwanza ni muhimu.  
-kliniki zihudhuriwe na wazazi wote wawili.

Hoja zozote 5× 1 =5

Mtiririko 1 =1

6

- (b) -Kliniki mazazi hupewa habari kuhusu maradhi ya watoto.
- Pia maradhi sugu
- Maradhi pia husababishwa na hali mbaya ya mama ua mazingira machafu.
- Utapiamlo pia huua watoto sana
- Mzazi ayajue maradhi haya kwa kuhudhuria kliniki.
- Nchini Kenya changamoto ya afya ya watoto ni huduma za kimsimgi.
- Serikali inawasihiwazazi kuhudhuria kliniki.
- Kuna utoaji wa chanjo za bure mashinani
- Gharama za huduma zimepunguzwa na ubora kuimarishwa.
- Serikali zinawapa mafunzo waliojitlea kutoa huduma za afya.
- Aidha kampeni za nyumba kwa nyumba zimeimarishwa.

$$\begin{aligned} \text{Hoja zozote}(8 \times 1) &= 8 \\ \text{Mtiririko} &= \frac{1}{9} \end{aligned}$$

### 3. MATUMIZI YA LUGHA

- (a) (i) hitilafiana,kosana,pingana  $(1 \times 1) = 1$
- (ii) anza  $(1 \times 1) = 1$

Tanbihi: Mtahini ahakiki sentensi

- (b)

S									
S <sup>1</sup>				U	S <sup>2</sup>				
KN	KT				KN	KT			
$\theta$	T	N	V		N	T	N	V	
$\frac{1}{2}$	Amejenga	Nyumba	nzuri	lakini	Kombo	Amejenga	Nyumba	ndefu	
$\frac{1}{2}$	$\frac{1}{2}$	$\frac{1}{2}$	$\frac{1}{2}$	$\frac{1}{2}$	$\frac{1}{2}$	$\frac{1}{2}$	$\frac{1}{2}$	$\frac{1}{2}$	

$$(8 \times \frac{1}{2}) = 4$$

- (c) (i) kutanguliza maelezo ya ziada kuhusu kitu kilichotajwa.  
Mf: Walipofika mkahawani waliagiza vyakula mbalimbali – dagaa,wali,biriani,pure na maharagwe.
- (ii) kuonyesha usemi unaodhiihirishwa na mtu Fulani  
Mf: Uasalma utaimarishwa nchini kote – Uhuru
- (iii) Kutanguliza na kumalizia maelezo ambayoyanaingia katikati ya isemi Fulani.  
Mf: Timu zile zote za soka – zilizokuwa zikifanya mazoezi uwanjani Nyayo – zimeondoka.  $(3 \times 1) = 3$

- (d) Wa – mafimu ya Nafsi  $\checkmark \frac{1}{2}$   
tu –mtendwa  $\checkmark \frac{1}{2}$   
pik – shina/mzizi  $\checkmark \frac{1}{2}$   
i –kiendelezi  $\checkmark \frac{1}{2}$   
a –kiishio  $\checkmark \frac{1}{2}$   
o - kirejeshi  $\checkmark \frac{1}{2}$

$$(6 \times \frac{1}{2}) = 3$$

- (e) kwa miguu (1 × 1)=1  
(f) (i) sh (1 × 1)=1  
(ii) b (1 × 1)=1
- (g) Mkikesha mtasinzia darasani na hamtasoma vizuri. (1 × 2)=2
- (h) (i) ala/kitumizi  
(ii) mahali (2×1)=2
- (i) (i) mf:miliki ————— milki  
tahadhari ————— nadhari (1 × 1)=1  
(ii) recodi -rekodi  
hesabu – hesabu  
hukumu – hukumu  
dai – dai  
Sumu – sumu (1 × 1)=1
- (j) changizo ni kielezi (1 × 2)=2  
TANBIHI –Mtahini ahakiki sentansi
- (k) Viunganishi vinavyoleta dhana ya changuo  
Mf:utakuja au hujui?  
Mtakula kwanza ama mtaoga kwanza sidhani yeye wala mwalimu. (2 × 1)=2
- (l) (i) Huonyesha dhamira dhahiri au kitendo hicho kinaendelea wakati huu.  
Mf: Itabidi umsubiri kwani bado ala.  
Mtoto yuko wapi? Achaza na wengine. (1 × 1)=1
- (ii) Huonyesha nomino iliyotajwa ina mazoea ya kutenda kitendo hicho.  
Mf:Je,Roni alifunga mabao.Ndio yuafunga.  
Alima shamba kila siku ili apate riziki.(1×1)=1
- (iii) Katika vichwa vyatubaki  
Mf:waziri atimuliwa kazi.
- (m) (i) kampuni yao imefilishwa na ufisadi. (1 × 1)=1  
(ii) Amedharauliwa na wenzake tangu siku hiyo. (1×1)=1
- (n) (i) Fahamu daima kwamba nawe hafi nawe.  
-Kuonyesha ufupisho wa nafsi ya kwanza. (1 × 1)=1  
(ii) Alikaripiwa na mamake alipokosa.  
-Inaonyesha kitendo kimefanywa na nani. (1 × 1)=1

- (o) Bi Keti alimwomba Batu amwangalilie nyumba hadi atakaporudi kwani alikuwa  
ameitwa kituo cha polisi na hakujua angerejea lini.  $(1 \times 2)=2$

- (p) vipasho vya lugha

-sauti → silabi → neno → sentensi

Mf:m → me → meno →

$(4 \times \frac{1}{2})=2$

- (q) k-konsonanti

I –Irabu

KIKKKI – mf:Jangwa  $(1 \times 1)=1$

kkkiki – mf: mbweha  $(1 \times 1)=1$

- (r) jitwana hili liliwabeba majanaya kidudu kisha yakafungua jiduka.  $(1 \times 2)=2$

- (s) kama huwabughidhi wanawake hujidinishi.  $(1 \times 1)=1$

#### 4. ISIMUJAMII

- (i) kuwepo kwa lahaja nyingi za Kiswahili.
- (ii) haja ya kuwa na lugha moja ya mawasiliano na elimu.
- (iii) maandishi yalikuwa tofauti hasa kutoka kwa wamisheni.Hivyo kukawa kuna haja ya kusawazisha maandishi ya kitaalamu.
- (iv) Shughuli za kidini ziliendeleshwa na madhehebu mbalimbali.Biblia na vitabu vya nyimbo vilitafsiriwa kwa lahaja mbalimbali,hivyo kuzua haja ya usawazishaji.
- (v) Hati tofauti zilitumiwa kukiandika Kiswahili.Hati zilizotumika ni kama vile za kiarabu na kirumi jambo lililosababisha namna tofauti za kuendeleza maneno hivyo kusanifisha Kiswahili kitoe aina moja.

# MTIHANI WA SHULE ZA UPILI WILAYA YA MARAKWET MAGHARIBI -2015 (MAWESSE)

*Cheti cha kuhitimu Elimu ya Sekondari Nchini Kenya (K.C.S.E)*

102/3

## KISWAHILI

### Karatasi 3

#### MWONGOZO WA KUSAHIHISHA INSHA

#### UTANGULIZI

Karatasi hii imedhamiria kutathmini uwezo wa mtahiniwa wa kuwasiliana na msomaji na kuwasilisha ujumbe kimaandishi,akizingatia mada aliyopewa .Mawasiliano haya yanategemea ukwasi wa lugha ya mtahiniwa, kwa mfano, kutunga sentensi sahihi zenyenye mtiririko mzuri kimawazo, lugha ya kuvutia na yenye mawazo asili , ubunifu mwingi na hati nadhifu.Kwa ketegemea maagizo ya swali lenyewe na umahiri wa lugha,ni lazima kutilia mkazo mtindo ,mada na uwezo wa mtahiniwa kufuata maagizo vilivyo .Mtaahiniwalazima aisome insha yote huku akizingatia sarufi, hoja ,msamiati ma mtindo ili aweze kuikadhiri kwa kurejelea viwango mbalimbali vilivyo pendekekezwa.Viwango vyenyewe ni A,B'C na D kutegemea uwezo wa mtahiniwa.

#### VIWANGO MBALIMBALI

#### KIWANGO CHA D KWA JUMLA MAKI 01-05

1 Insha haieleweki kwa vyovyote vile ama uwezo wa mtahiniwa wakutumia lugha ni hafifu sana , hivi kwamba mtahini lazima afikirie kile mtahiniwa anacho jaribu kuwasilisha.

2 Mtahiniwa hana uwezo wa kutumia maneno ya Kiswahili kwa njia inayofaa

3 Lugha imevurukgika ,uakifishaji na insha ina makosa ya kila jaina.

4 Kujitungia swali na kulijibu

5 Insha ya urefu wa robo ikadiriwe hapa

#### NGAZI MBALIMBALI KIWANGO CHA D

#### D-(D YA CHINI) MAKI 01-02

1 Insha haina mpangilio maalum na haieleweki kwa vyovyote vile

2 Kujitungia swali tofauti na kulijibu

3 Kuandika kwa lugha isiyo Kiswahili au kuchanganyika ndimi.

4 Kunakili swali au maswali na kuyakariri

5 Kunakili swali au kichwa tu

#### D WASTANI MAKI 03

1 Mtiririko wa mawazo haupo

2 Mtahiniwa amepotoka kimaudhui.

3 Matumizi ya luugha ni hafifu mno

4 Kuna makosa mengi ya kila aina

#### D+ (D YA JUU) MAKI 04-05

1 Insha ya aina hii huwa na makosa mengi ya kila aina .Lakini unaweza kutambua kile ambacho mtahiniwa anajaribu kuwasilisha

2 Hoja hazikukuelezwu kikamilifu / mada haikukuzwa ilivyo.

3 Mtahiniwa hana uhakika wa matumizi ya lugha.

4 Mtahiniwa hujirudiarudia

5 Insha vyenyewe urefu wa nusu ikadiriwe hapa.

#### KIWANGO CHA C KWA JIJMLA MAKI 06-10

1. Mtahiniwa anajaribu kuishughulikia rnada japo hakuikuza na kuiendeleza vilivyo.

2. Mtahiniwa anawasilisha ujunibe kwa njia isiyovutia /hana ubunifu wa kutosha.

3. Mtahiniwa anaakifIsha seatensi vibaya.

4. Mtiririko wa mawazo unaanza kujitokeza japo kwa njia hafifu.

5. Insha ina makosa mengl ya sarufi, ya nisamiati na ya tahajia (hijai.)

6. Insha yeny e urefu wa nusu ikadiriwe hapa.

### **NGAZI MBALIMBALI ZA KIWANGO CHA C**

#### **C- (C YA CHINI) MAKI 06-07 .**

1. Mthiniwa ana shida ya kuwasilisha na kutiririsha mawazo yake.

2. Mtahiniwa hana msamiati wa kutosha wala miniundo ya sentensi ifaayo.

3. Mtahiriwa ana.fanya makosa mengi ya sarufi, ya hijai na ya msarniati na insha yake haieleweki kwa urahisi.

#### **C WASTANI MAKI 08**

1. Mtahiniwa anawasilisha ujumbe lakini kwa njia hafifu,

2. Dhana tofautitofauti hazijitokezi wazi.

3. Mtahjniwa hana ubunifu wa kutosha.

4. Mtiririko wa mawazo ni hafifu na hana-ufundi wa lugha unaofaa.

5. Amejaribu kuishughulikia mada a1iyopewa

6. Mtahiniwa ana shida ya uakifishaji.

7. Mtahiniwa *anafanya* makosa mengi ya sarufi ya hijai na ya msamiati lakini bado insha inaeleweka. .

#### **C+ (CYAJUU) MAKI 09-10**

1. Mtahiniwa anawasilisha ujumbe vizuri akizingatia mada lakini kwa *njia* isiyo na mvuto.

2. Dhana tofautitofautj zinajitokeza japo kwa njia hafifu.

3. Kuna mtiririko wa mawazo japo hana ufundi va lugha unaofaa.

4. Misenio na methali zimetumika kwa njia hafiu.

5. Ana shida ya uakifishaji.

6. Kuna makosa ya sarufi, ya msamiati na ya hijai yahayoathiri mtiririko wa mawazo.

### **KIWANGO CHA B KWA JUMLA MAKI 11-15**

1. Katika kiwango hiki, mntahiniwa anaonyesha hali ya kuimudu lugha.

2. Mtahiniwa anatumia miundo tofauti tofauti ya sentensi vizuri.

3. Mtahiniwa ana uwezo wa kutumia lugha kwa ufasaha.

4. Mada imekuzwa na kuudelezwa kikamilifu.

5 Insha ya urefu wa robo tatu ikadiriwe katika kiwango hiki.

### **NGAZI MBALIMBALI ZA KIWANGO CHA B**

#### **B-(B YA CHINI) MAKI 11-12 -**

1. Mtahiniwa anawasilisha ujumbe *vizuri* kwa kueleza hoja tofautitofauti akizingatia mada.

2. Mtahiniwa ana mtiririko mzuri wa nawazo.

3. Mtahiniwa anatumia mifano michache ya msamiati unaovutia.

4. Makosa yanadhthirika/kiasi

#### **B WASTANI MAKI 13**

1. Mtahiniwa anadhihirisha hali ya kuimudu lugha

2. Mawazo ya mtahiniwa yanadhihirika akizingatia mada.

3. Mtahiniwa anateua na kutumia mifano michache ya misamiati mwafaka.

4. Sarufl yake ni nzuri.

5. Makosa ni maachache/kuna makosa machache.

#### **B+ (B YA JUU) MAKI 14-15**

1. Mawazo ya mtahiniwa yanadhihirika na anajieleza waziwazi.

2. Mtahiniwa anawasiliha ujumbe kwa njia inayovutia na kwa urahisi akizingatia mada.

3. Mtahiniwa ana mchanganyiko mzuri wa msamiati miaovuti unaovutia.

4. Sarufl yake ni nzuri.

5. Uakifishaji wa sentensi zake ni mzuri.

6. Makosa ni machache ya hapa na pale.

### **KIWANGO CHA A KWA JUMLA MAKE 16-20**

1. Mtahiniwa ana ubunifu wa mawazo yanayodhihirika na kutiririka akizingatia mada.

2. Mtahiniwa anadhihirisha ujuzi wa lugha yeny e mnato.

3. Ana uwezo wa. kutumia tamathali za usemii ili kutoa hisia zake kwa njia bora na kwa urahisi.
4. Umbuji wake unadhihirisha ukomavu na ukakamavu wake kimawazo.
5. Insha ina urefu kamili.

### **NGAZI MBALIMBALI ZA KIWANGO CHA A**

#### **A- (YA CHINT) MAKI 16-17**

- I. Mtahiniwa anadhihirisha ukomavu wa lugha.
2. Mawazo ya mtahiniwa yanadhihirika na anashughulikia mada.
3. Ana mtiririko mzuri wa mawazo
4. Msamiati wake ni mzuri na unaovutia.
5. Sarufi yake ni nzuri.
6. Anatumia miundo tofauti tofauti ya sentensi kiufundi.
7. makosa ni machache yasiyokusudiwa.

#### **A WASTAN MAKI 18**

1. Mtahiniwa anawasilisha ujumbe vizuri kulingana *na* mada.
2. Anajieleza kikamilifu akitumia lugha ya mnato/kunasa.
3. Anatoa hojazilizokomaa.
4. Anatumia msamiati wa hali ya juu na unaovutia zaidi.
5. Anatumia miundo tofauti tofauti ya sentensi kiufundi.
6. Makosa ni nadra kupatikana.

#### **A+(AYAJUU)MAKI 19 - 20**

1. Mawazo yanadhihirika zaidi na mada imeshughulikiwa vilivyo.
2. Anajieleza kikamilifu akitumia Iugha ya mnato.
3. Hoja zake zimekomaa. na zinashawishi.
4. Msamiati wake ni wa hali ya juu na unaovutia zaidi
5. Sarufi yake ni nzuri zaidi/kabisa.
6. Anatumia ntiundo tofauti tofauti ya senteusi kiufundi.
7. Makosa yote kwa jumla hayazidi matano.

### **VIWANGO MBALIMABLI KWA MUHTASARI**

KIWANGO	NGAZI	MAKI
A	A+	19 -20
	A	18
	A-	16 - 17
B	B+	14 – 15
	B	13
	B-	11 - 12
C	C+	09 – 10
	C	08
	C-	06 - 07
D	D+	04 – 05
	D	03
	D-	01 - 02

### **USAHISHAJI NA UTUZAJI KWA JUMLA**

Mtahini ni sharti aisome insha yote akizingatia vipengee muhimu. Vipengee hivi ni maudhui, msamiati, mtindo, sarufi na hijai.

#### **MADHUI**

1. Maudhui ni hoja au mambo yanayozungumziwa, kuelezewa *au* kuhadithiwa kwa mujibu wa mada iliyoteuliwa.
2. Maudhui ndio hasa uti wa mgongo wa insha yoyote ile.
3. Ubunifu wa mtahiniwa hukisiwa kwa kutathmini uzito wa maudhui yake kulingana na mada teule.

#### **MSAMIATI**

Msamiati ni jumla ya maneno yatumiwayo katika lugha husika, Mtahinwa anatarajiwa kutumia msamiati unaooana na mada teule. Kutegemea ukwasi wa lugha alionao, mtahiniwa anatarajiwa kuikuza mada kwa

kuifinyanga lugha kiufundi. Ni muhimu kuelewa kwamba kutokana na maendeleo na ukuaji wa teknolojia na mawasiliano, maneno mapya yanaibuka kila uchao.

## MTINDO

Mtindo unahusu mambo yafuatayo.

- Mpangilio wa kazi kiaya.
- Mtiririko na mshikamano wa mawazo kiaya na katika insha nzima.
- Hati nzuri na inayosomeka kwa urahisi.
- Matumizi ya tamathali za userni, kwa mfano, methafi, misemo, jazanda na kadhalika.
- Kuandika herufi vizuri kwa mfano Jj, Pp. Uu, Ww na kadhalika.
- Sura ya insha.
- Unadhifu wa kazi ya mtahiniwa.

## SARUFI

Sarufi ndio msingi wa lugha. Ufanisiwa mawasiliano hutegemea uwezo wa mtahiniwa wa kutunga sentensi sahihi zenye uwiano wa kisarufi. Mtahini ataonyesha makosa yote ya sarufi yake katika insha anayosahihisha. Makosa ya sarufi huweza kutokea katika:

- (i) Matumizi ya alama za uakifishaji.
- (ii) Kutumia herufi kubwa au ndogo mahaii pasipofaa.
- (iii) Matumizi yasiyofaa ya ngeli na viambishi, viunganishi, nyakati, hali, vihusiano na kadhalika.
- (iv) Mpangilio wa maneno katika sentensi.
- (v) Mnyarnbuliko wa vitenzi na majina.
- (vi) Kuacha neno linalohitajika au kuongeza neno lisiohitajika katika sentensi.
- (vii) Matumizi ya herufi kubwa:
  - a, Mwanzo wa sentensi
  - (c) siku za juma,mwezi n.k.

### b,Majina ya pekee.

- i) Majina ya mahali, mji, nchi, mataifa na kadhalika.
- ii) Mashirika, masomo, vitabu n.k.
- iii)makabila, lugha nk.
- vi)Jina la Müngu.
- v) Majina ya kutambulisha hasa wanyama wa kufugwa, kwa mfano yale ya mbwa- F popi, simba, Tomi na menineyo
- vi)majina ya watu (binadamu)

## MAKOS YA HIJAI/TAHAJIA

Haya ni makosa ya maendelezo. Mtahini anashauriwa asahihishe huku akiyaonyesha yanapotokea kwa mara ya kwanza tu. Makosa ya tahajia huweza kutokea katika:

- (a) Kuteaganisha neno kwa mfano ‘aliye kuwa’
- (b) Kuunganisha maneno kwa mfano ‘kwasababu’.
- (c) Kukata silabi visivyo afikapo pambizoni kama vile ‘ngan – o’
- (d)Kuandika herufi isiyofaa kwa mfano ‘ongesa’ badala ya ‘ongeza’
- (a) Kuacha herufi katika neno kwa mfano ‘aliekuja’ badala ya ‘aliyekuja’.
- (f) Kuongeza herufi isiyohitajika kama vile ‘piya’ badala ya ‘pia’.
- (g) Kuacha alama inayotarajiwa katika herufi kama vile j i.
- (11) Kukosa kuandika kistari cha kuendelezea neno afikiapo pambizoni au kukiandika mahali pasipofaa.
- (i). Kuacha ritifa4 au kuiandika mahali pasipofaa, kwa mfano ngombe, ngom’be, n’gombe, ng’mbe.n.k
- (j) Kuandika maneno kwa kifupi kama vile k.v., k.m., .y.v., n.k. na kadhalika.
- (k) Kuandika tarakimu kwa mfano 27-08-2010.

## ALAMA ZA KUSAHIHISHIA

— Hupigwa chini ya sehemu ambapo kosa la sarafi limetokea kwa mara ya kwanza tu .

— Hupigwa chini ya seheniu au neno ambapo kjisa Ia hijai imetokea kwa mara ya kwanza tu.

✓ Hutumiwa kuonyesha hoja inapokamilikia pambizoni kushoto.

✗ Hutumiwa kuonyesha kuachwa kwa neno/maneno.

✓ Hutumiwa kuonyesha msamiati bora. Alama hii hutiwa juu ya neno lenyewe.

X Huturniwa kuonyesha msarniati usiofaa. Alam'a hii hutiwa juu ya nerto lenyewe.

Maelezo mafupi yanahitajika kuhusu tuzo lililotolewa. Kila ukurasa uwe na alama ya katikati ili kuthibitisha kuwa mtahini ameupitia ukurasa huo.

## UKADIRIAJI WA UREFU WA INSHA

Maneno 9 katika kila msitari	1 ½ ukurasa mmoja na nusu.
Mañeno 8 katika kila msitari	1 ¾ ukurasa mmoja na robo tatu
Maneno 7 katika kila msitari .	2 kurasa mbili
Maneno 6 katika kila msitari	2 ¼ kurasa mbili na robo
Maneno 5 katika kila msitari	2 ¾ kurasa mbili na robo tatu.
Maneno 4 katika kila msitari	3 ¾ kurasa tatu na robo tatu.
Maneno 3 katika kila msitari	4 ½ kurasa nne na nusu.
Kufikia maneno 174	Insha robo
Maneno 175- 274	Insha nusu
Maneno 275 – 374	Insha robo tatu
Maneno 375 na kuendelea	Insha kamili